

# YA BIASHARA

Mkataba huu umetokwa kuu mbili ambazo ni mpangishaji na mpangaji na makubaliano yafuata tarehe July 31 2025 kati ya

Ndugu **MANULIFE TRADING COMPANY LTD** wa **TABORA** ambae katika mkataba huu atajulikana kama mpangishaji / mwenye nyumba iliyopo ipuli - muhalitani Tabora Manispaa kwa upande mmoja



NA

Ndugu Damas John Tesha wa S.L.P 590 Tabora ambae katika mkataba huu atajulikana kama mpangaji wa nyumba iliyopo Ipuli - Muhalitani Tabora Manispaa kwa upande mwingine.

## **HIVYO BASI PANDE ZOTE MBILI (MWENYE NYUMBA NA MPANGAJI) WAMEKUBALIANA YAFUATAYO;**

**KWAMBA:** Mpangaji amekubali kulipa kodi yenye kiwango cha dola za kimarekani elfu moja mia moja tu (USD 1,100/-) kwa mwezi kwa miezi sita ya mwanzo.

**KWAMBA;** Mpangishaji amempangisha mpangaji nyumba kwa muda wa miezi thelathini na sita yaani miaka mitatu kuanzia tarehe ya kusainiwa mkataba huu.

**KWAMBA;** kwa kipindi cha miaka mitatu mpangaji anatakiwa kulipa kodi kwa vipindi vya miezi sita sawa na kwa miezi sita ya kwanza atalipa dola za kimarekani elfu sita mia sita tu (USD 6,600/-). Hivyo kwa muda wa miaka mitatu mpangaji atalipa kodi kwa vipindi vyamiezi sita (6) ambapo malipo yatategemea na hali halisi ya soko kwa miezi sita inayolipiwa.

**KWAMBA;** Mpangaji atawajibika kulipa gharama nyingine zote kama Ankara za maji, umeme, malipo ya wafanyakazi, ulinzi, na usafi pamoja na kufuata utaratibu utakaowekwa na mwenye nyumba kwa maslahi ya jamii inayomzunguka pamoja na utunzaji wa nyumba.

**KWAMBA;** Mpangaji atafanya ujenzi wa nyumba kwa nje kwa matumizi yake binafsi na **HAYAHUSIANI** na gharama za ulinzi kodi kulingana na mkataba huu.

**KWAMBA;** Mpangaji haruhusiwa kumpangisha mtu mwingine na kuchukua kodi na mwenye nyumba akibaini mpangaji kufanya hivyo kutamfanya mpangaji kujiondoa katika haki yake ya kumiliki nyumba mara moja.



**KWAMBA; Mpangaji** harusiwi kufanya biashara za magendo au ambazo haziruhisiwi kisheria na ikibainika hatua za kisheria zitachukuliwa na mpangaji kuchia nyumba mara moja.

**KWAMBA; Kwa mpangaji** atawajibika kwa ulinzi na usalama wa mali zake na mwenye nyumba hatohusika na upotevu wa mali yoyote itakayokuwa nje au ndani ya nyumba.

**KWAMBA; Mpangaji** haruhusiwi kufanya marekebisho ya aina yoyote ndani ya nyumba bila kumpa taarifa mwenye nyumba kwa maandishi.

**KWAMBA; Mpangaji** atanunua eneo pamoja na nyumba iliyoko eneo la kiwanja ndani ya mwaka mmoja na kama atashindwa atatakiwa kurejesha nyumba katika hali aliyokuta

**KWAMBA; Malipo** yafanyike kupitia akaunti number 0152364461100 in name of Damas John Tesha.

**KWAMBA; Kodi** ya miezi sita ya kwanza itaanza 01/08/2025 na itaishia 30/01/2026.

## **IELEWEKE MKATABA HU NI HIARI ICHUKULIWE KUWA HALALI YA SHERIA**



JINA LA MWENYE NYUMBA

**DAMAS J. TESHA** SAHIHI

SHAHIDI WA MWENYE NYUMBA **OSWALD AMAN KABANA**

SAHIHI

JINA LA MPANGAJI

SAHIHI

SHAHIDI WA MPANGAJI

SAHIHI

